

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MABADILIKO YA TOZO ZA UZIDISHAJI UZITO WA MAGARI**

Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) inapenda kuutaarifu Umma wa Watanzania hususan, Wasafirishaji na wadau wetu wote kwamba, ukomo wa viwango vya tozo ya uzidishaji uzito wa magari vinavyotumika sasa ni tarehe 31 Desemba, 2020. Hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Udhhibiti wa Uzito wa Magari ya mwaka 2016 (The East African Community Vehicle Load Control Act, 2016) na kanuni zake.

Hivyo, mnajulishwa kuwa, kuanzia tarehe **01 Januari, 2021**, viwango vipya vya tozo za uzidishaji uzito wa magari vitaanza kutumika kama vilivyoainishwa kwenye Jedwali la tatu la Kanuni za Taratibu za Usimamizi za mwaka 2018 (The East African Community Vehicle Load Control (Enforcement measures) Regulations, 2018).

Aidha, Sheria na Kanuni zinazohusu viwango vipya vya tozo za uzidishaji uzito wa magari zinapatikana kupitia tovuti ya Wizara [www.mwtc.go.tz](http://www.mwtc.go.tz).

Kwa taarifa hii, napenda kuwahimiza na kuwashauri wadau wote kujiandaa kwa utekelezaji wa mabadiliko hayo.

Imetolewa na;

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Elius A. Mwakalinga'.

Arch. Elius A. Mwakalinga

**KATIBU MKUU – SEKTA YA UJENZI**

18 Novemba, 2020